

Want to see Your
BANNER
HERE?

[Click Here](#)

[Mwanzo](#)

[Habari](#)

[Biashara](#)

[Michezo & Burudani](#)

[Maoni Ya Mhariri](#)

[Safu](#)

[Makala](#)

28 FEB
2018

HELLEN MWANGO

HABARI
(/SW/SECTION
/HABARI)

Nipashe

AG aomba kizuizi wachezesha upatu

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), amefungua maombi mahakamani dhidi ya walalamikiwa watatu, Jones Moshi, James Gathonjia na Kampuni ya Refaro Afrika Limited ya kuzuia walalamikiwa kutojijhusisha na fedha zilizopo kwenye akaunti ya kampuni hiyo zilizopatikana kwa mchezo wa upatu.



MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI DKT. ADELARDUS KILANGI.

Aidha, AG anaiomba Mahakama ya Hakim Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, kuwazuia walalamikiwa kujihusisha kwa namna yoyote na fedha zilizopo kwenye akaunti ya Kampuni ya Refaro Afrika Limited iliyopo Benki ya Biashara ya Kenya (KCB), tawi la Mlimani City.

Maombi hayo yamepangwa kusikilizwa mbele ya Hakim Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Katika maombi hayo yaliyoungwa mkono na kiapo cha Wakili wa Serikali Mwandamizi, Shadrack Kimaro, mkuu huyo wa usimamizi wa sheria nchini anaiomba mahakama kumwamuru Meneja wa KBC tawi la Mlimani City kutowaruhusu kutoa, kuhamisha, kujishughulisha kwa namna yoyote na akaunti hiyo.

Dia alidai kuwa walalamikiwa wa kwanza na wa pili wako chini ya uchunguzi wa kosa la kula niama

na kuendesha upatu, unaoendelehwa Jeshi la Polisi.

Kwa mujibu wa kiapo hicho, mlalamikiwa wa kwanza Moshi ni mfanyabiashara na mkazi wa Mbezi jijini Dar es Salaam, Gathonja ni mkazi wa Nairobi nchini Kenya na wa tatu ni kampuni iliyosajiliwa yenye ofisi zake Kijitonyama.

Mlalamikiwa wa kwanza na ya pili ni wanahisa na wakurugenzi wa kampuni hiyo na iliposajiliwa ilipata leseni ya kufanya biashara wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa maombi hayo, kampuni hiyo ilipata leseni ya biashara ya vocha za simu na vifaa vya simu za mkononi.

Aidha, imedaiwa kampuni hiyo ilianza kuhamasisha watu kujiunga kama wasambazaji wa muda wa maongezi kwa njia ya matangazo na semina.

"Wanachama walitakiwa kujiunga na kulipa Sh. 128,500 na fedha hizo ziliingizwa moja kwa moja kwenye akaunti ya kampuni... wanachama waliojiunga walipewa majukumu ya kutafuta wanachama wapya kwa kulipwa bonasi ya Sh. 20,000," ilidaiwa kupitia maombi hayo na kuelezwa zaidi:

"Wale ambao walifanikiwa kuvuta wanachama wengi zaidi wangeshinda zawadi ya gari, nyumba au Kiwanja... Kwa muonekano wa biashara hiyo, huo ni upatu na kampuni hiyo ilifanikiwa kupata wanachama 12,956 baada ya kulipa kiingilio hicho," alidai AG kupitia maombi hayo.

Maombi hayo yamepangwa kusikilizwa Machi 12, mwaka huu.





[Next \(/sw/habari/ashikiliwa-nolisi-kwa-tuhuma-za-kuhaka-](/sw/habari/ashikiliwa-nolisi-kwa-tuhuma-za-kuhaka-)

HABARI KUBWA



[DC atangaza msako nyumba kwa nyumba waliokeketwa \(/sw/habari/dc%20atangaza-msako-waliokeketwa-nyumba-kwa-nyumba\)](/sw/habari/dc%20atangaza-msako-waliokeketwa-nyumba-kwa-nyumba)



[Mafataki watangaziwa kiamia \(/sw/habari/mafataki%20watangaziwa-kiaama\)](/sw/habari/mafataki%20watangaziwa-kiaama)



[Ufaulu kiduchu wamzindua Jafo, atoa tamko \(/sw/habari/ufaulu-kiduchu-wamzindua-jafo-atoa-tamko\)](/sw/habari/ufaulu-kiduchu-wamzindua-jafo-atoa-tamko)



[Ajirusha baharini kina kirefu safarini Z'bar \(/sw/habari/ajirusha%20baharini-kina%C2%A0-kirefu-safarini-zbar\)](/sw/habari/ajirusha%20baharini-kina%C2%A0-kirefu-safarini-zbar)